MOMBASA COUNTY ASSEMBLY

HANSARD REPORT

Wednesday, 13th July, 2016

The House met at 2.36pm.

(Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid) in the Chair)

PRAYERS

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Hon. Members you may have your seats, Yes Clerk.

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

Yes Hon. Members I have a letter coming from the Office of the Leader of the Majority and it says;

(*Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid) read Communication)*

"Confirmation in appointment, to the position of County Assembly Clerk. The County Assembly Service Board (CASB) vide their meeting held on 12th July, 2016, resolved under Min. No 1/CASB/12th July 2016, that the position of County Assembly Clerk be filled and that the current Acting County Assembly Clerk be confirmed into the position of County Assembly Clerk.

This is therefore to communicate the matter to you so that the officer can be vetted and approved as per the Law".

(Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid) ended Communication)

(Applause)

Now, for this affair I now direct to the Committee of the Appointment to work on it.

(Applause and Laughter)

Yes Clerk

STATEMENT

Port Ritz Ward MCA,

(Provision of a designated passage at Likoni Ferry for School Children)

Hon. Mwalimu: Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi nimesimama kuwa niko na maoni; ningependa kuelezea Nyumba hii na pia vile vile ningependa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchukuzi waweze kuja katika Nyumba hii na aelezee Nyumba hii yanayowasibu watoto wa shule wanaovuka katika kivuko cha Likoni Ferry.

Mheshimiwa Spika mimi naomba kupitia Nyumba hii kuna watoto ambao ni wadogo; la pili wengi huwa ni wa shule wanapovuka katika kivuko cha Likoni Ferry huwa wanachanganywa pamoja na watu wazima.

Wengine Mheshimiwa Spika huwa kuna watu wale ambao huwa na mizigo mizito, hususan wakati wa asubuhi na wakati wa jioni.

Mimi naomba Mheshimiwa Spika watoto wale waweze kuangaliwa, wapewe hadhi watoto wale na watengewe sehemu ambayo watakuwa wakivuka bila bugdha.

Kwa sababu wanapitia majanga, wanapitia uzito Mheshimiwa Spika na ni watoto wetu kwa sababu wanapitia majanga, wanapitia mazito na ni watoto wetu na twaelewa haswa ni watoto wa shule, watoto ambao wanaenda kutafuta elimu.

Mheshimiwa Spika tusipowalinda watoto wale leo tujue tutawakosa kesho na mtoto amerauka asubuhi anapatana na dharubu anarudi jioni anapatana na dharubu hiyo inachangia kwa masomo yao kushuka chini kwa sababu zile dharubu wanazopitia pale feri.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ningependa kuomba Mwenyekiti wa Kamati ya Uchukuzi achukulie jambo hili kwa uzito na ikiwezekana kupitia kwa Kiti chako wewe ndiye utakayetuelekeza kupitia kwa kiti chako ikiwa ataweza kwenda kuongea ama Kamati nzima iende iongee watoto wawe wanaangalia vizuri katika kivuko kile.

Mheshimiwa Spika iko labda vile wanaangaliwa lakini mimi nasema hawaangaliwi vizuri; twataka wavuke pale bila bugdha, twataka wakifika Mheshimiwa Spika wanachukuliwa kama vile almasi maana ndio almasi zetu…

(Laughter)

Mheshimiwa Spika mimi naomba wenzangu wa Bunge hili tushirikiane pamoja tuangalie maslahi ya watoto wetu maana pale Likoni Ferry utakuta mtoto ndogo labda hata darasa la tatu akiwa anaenda kupanda ama kushuka feri zile anapatana na ma *bouncer* wakubwa ambao wakimuona anaenda njia ambayo kidogo hawezi kuvuta pumzi mtoto kama yule unaona akisukumwa anaelekezwa sehemu ile ambayo ina watu wengi.

Watoto hata kuvuta pumzi kwao inakuwa ni dhiki, Mheshimiwa Spika mimi nawaomba wenzangu tushirikiane pamoja na tusukume hio Kamati ya Uchukuzi jambo hili ilichukulie kwa dharura sana. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Mheshimiwa Amur.

Hon. Amur: Ahsante Bwana Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Fadhili amekuja na wazo zuri lakini Kenya bado iko ukoloni mambo leo; nikisema Kenya ni ukoloni mambo leo….

(Interruption)

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Hon. this is a statement and a statement usually is not debated unless someone asks the House if the House is of the opinion that the statement should be debated.

Hon. Amur: But I just have something to add, something Mr. Speaker.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** It's a statement somebody must ask the House, the House must agree so that the statement can be debated.

Hon. Amur: Thank you Mr. Speaker.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Yes Hon. Fadhili?

Hon. Mwalimu: Ahsante Mheshimiwa Spika kupitia kiti chako kulingana na uzito wa jambo hili na *Standing order* zetu zaruhusu ikiwa utaruhusu hata kama ni watu wawili watatu wachangie ili tupate uzito lakini sio vile Mheshimiwa Amur anavyo pinga, la Mheshimiwa Spika tupate uzito wa jambo hili ili Kamati na nakurai Mwenyekiti wa Kamati ya Uchukuzi Mheshimiwa Amir Thoya yuko hapa ndani…..

(Applause)

Atajuwa pia anapokwenda kule, atakuwa anabeba uzito gani.

Mimi nimesema labda swala moja labda pia twaweza kuongezea maswala mengine mawili matatu yakaeza kuifanya shughuli hii ikawa ni nzito zaidi.

(Question put and agreed to)

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Hon. Amur you can now continue.

Hon. Amur: Mheshimiwa Spika nilikuwa nasema Kenya bado kuna ukoloni mambo leo wakati gari zikivuka pale zikibeba watalii, watalii hawateremshwi lakini hizo gari zikibeba warabu ama Mkenya mwenzangu anateremshwa akiwa juu na mtu huyo anaenda safari pengine anaenda Tanzania ama Ukunda na gari ya kibinafsi.

Kama gari za kwenda Tanzania zinateremshwa wamama watu wazima wanakua *subjected to the rate* ambayo wageni ambao ni watalii wanapewa hii ni kubagua ikiwa gari zote za abiria zinateremsha watu.

Basi mimi ningeomba na hii pia ichangiwe kwamba gari zote hata za watalii wakija wateremke kama kila mtu atakiwa kuteremka, ikiwa watalii wanakubaliwa basi hata wenyeji ambao wanasafiri kwa usafiri pia hao wateremshwe. Ahsante Mheshimiwa Spika.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Yes Mheshimiwa Mary Akinyi.

Hon. (Ms.) Akinyi: Ahsante Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na dukuduku ama wazo kwa sababu jana tulipokuwa katika *House Business* kulikuwa na Mswada juu ya ajali kwa Feri ambayo huo Mswada ulikuwa uletwe na Mheshimiwa Amir Thoya.

Sasa Mheshimiwa nashangaa ndio ni mambo ya Feri na pia hata ukiwa unaangalia yale mambo ambayo vile Mheshimiwa Fadhili amechangia unaona tu ni kama inakaribia ule mjadala ambao ulikuwa uletwe katika Jumba hili na Mheshimiwa Amir Thoya.

Kwa hivyo mimi Mheshimiwa ningeomba ule mjadala ambao ulikuwa uletwe na Amir Thoya leo hii wakati kama huu katika Bunge Amir Thoya alete ule mjadala wake tuendelee nao tuweze kuweka mambo haya ambayo Mheshimiwa Fadhili amekuja nayo ya kupakata watoto hata wanapo vuka hata wanapo pita hapo. Ahsante Mheshimiwa Spika.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Hon. Amir Thoya has not brought his Motion and Hon. Amir Thoya you will table it. Yes Hon. Ibrahim Kondo.

Hon. Ibrahim Kondo: Ahsante Mheshimiwa Spika, suala lililoletwa mbele ya Nyumba hino lina umuhimu kwa kizazi kinacho kuja; kwanza kabisa ni jambo la busara kwa Nyumba hino kupitia kwa Kamati kwenda kukutana na kitengo che Kenya Ferry ambapo kuna Mwenyekiti mpya aliyeteuliwa juzi Mheshimiwa Ramadhan Kajembe ili masuala haya tuyaweke wazi na tubaini kwamba….kupita kwa watoto wetu yatatautilwa.

Mheshimiwa Spika kusema kweli watoto wetu wanatatizika katika kivuko cha Kenya Ferry ni mambo tunayaona; leo asubuhi nimekutana na kijana anayesoma maeneo ya Istiqama sehemu yake ya nyuma imechafuliwa kwa wale wanabeba mzigo.

Swala kama lile litafanya wanafunzi wawe hawana raha Mheshimiwa Spika, sisi ni wanadamu na hatuwezi kumkosea sisi tulivyoumbwa katika kivuko kilekile kuna wengine wana maumbo tofauti, watoto wetu wa shule basi kuna wale wameasi ukapera wanaanza kupata watoto wetu kwa nyuma ambavyo si jambo la busara….

(Laughter)

Ni kwa sababu ya kusukumwa pale ili kufaidi zile asali asali kidogo, kwa wale watoto Mheshimiwa Spika hili swala pia liko pale kwa kile kivuko pale Ferry na lina sumbua watoto wetu hata muda mwingine wakina mama juu wakatukana wazee ambao wanamaliza shughuli zao pale pale. Mheshimiwa Spika hili jambo ni la kusikitisha sana...

(Interruption)

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Ndio mheshimiwa wa Mwakirunge.

Hon. Mwinga: Mheshimiwa Spika mimi nashangazwa na Mheshimiwa ambaye ako kwa sakafu, la kushangaza ni kwamba yeye haishi upande wa Likoni, anajuaje haya mambo

yanatokea Mheshimiwa Spika? Ana udhibitisho ya kuwa haya mambo yanatokea Mheshimiwa Spika?

(Laughter)

Hon. Ibrahim Kondo: Mheshimiwa Spika Mheshimiwa wa Mwakirunge nataka afahamu anayeongea ni Mwenyekiti wa Biashara, Viwanda na Kawi katika mji wa Mombasa na ni Mheshimiwa ambaye anafanya kazi hawezi kulala hata nyakati za asubuhi Mheshimiwa huyu aliitwa kwa mambo ya biashara maeneo ya Likoni.

Kwa hivyo ni lazima afahamu kwamba mimi ni Mwenyekiti si lazima nilale kule ninaweza amka asubuhi nikaenda Uwanja wa ndege nikachukua *helicopter* nikatua Likoni hili ni jambo lipo na ni lazima afahamu …..

(Interruption)

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Yes Mheshimiwa wa Mjambere unasemaje?

Hon. Mwabashiri: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii nilikuwa nauliza swali ambalo ndugu yangu hajajibu ambayo hata Mheshimiwa wa Timbwani amesema habari hizo kwa miaka mingi na hajazipata…

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Habari zipi ziseme?

Hon. Mwabashiri: Hizi na gandia kina mama…

(Laugher)

Sasa swali ni je kama ni yeye anaketi nyuma ya kina mama na kufanya tabia hiyo aseme sasa asije akasema kuna watu na Mheshimiwa wa Timbwani anasema hajaona; kama yeye anasema sijui alfajiri sijui sokoni, kuna soko gani Likoni kama yeye anayajua masoko yote anafanya hizo shughuli alete hapa kwenye Bunge.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Mheshimiwa wa Timbwani ni kweli watu wanaibiwa mapenzi huko?

Hon. Ogalo: Mheshimiwa Spika hiyo ni mambo ya watu wa Kipevu, mimi natoka Likoni na Wodi yangu ndio inahusikana na hiyo Ferry na sijasikia tabia kama hiyo, kile nataka kusema nitawacha Mheshimiwa azungumze ndio nitamwambia mambo yangu.

Hon. Ibrahim Kondo: Mheshimiwa Spika ningelipenda kufahamisha Bunge hili ya kwamba mambo tunayoongea hapa ni mambo ya ushahidi na Mheshimiwa wa Timbwani tulimsaidia akapata kibali cha Ferry kitambo huwa havuki na pale…

(Laughter)

Mheshimiwa Spika mambo haya yako mpaka kwenye vyombo vya habari ziko kwa hivyo lazima atambue...

(Interruption)

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Mheshimiwa wa Timbwani wasemaje?

Hon. Ogalo: Mheshimiwa Spika mtu ambaye anasaidia mtu kupata kibali mbona yeye hana..

(Laughter)

Hon. Ibrahim Kondo: Mheshimiwa Spika swala la kibali kama kiongozi wa biashara ni jukumu langu kuwatetea Waheshimiwa; Mheshimiwa wa Timbwani mwenyewe alishtukia kibali amepewa katika ofisi hizi lakini hakujua ni kwa njia gani.

Kwa hivyo ningependa kumfahamisha ikiwa anataka kuona shughuli zikiendelea watoto wetu wanavyonyanyaswa ashuke kule atafute dereva akue kila siku akivuka kwa Ferry.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika hilo swala lililoletwa na Mheshimiwa Fadhili ina umuhimu watu wakae chini na viongozi wa Kenya Ferry waangalie watoto wale tutawaweka kwa mikakati gani wakati wanapovuka wakati wa asubuhi na ndugu yangu Mheshimiwa wa Mwakirunge ningependa kumsihi ajue ya kwamba wale ni watoto na tuna dhamana nao leo na hata kesho. Ahsante Mheshimiwa Spika.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Yes Hon. of Kazandani.

Hon. Mohamed Ndanda: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, hoja hii ni ya muhimu mimi nakubalina nayo na naiunga mkono na hoja hii Mheshimiwa imekuja wakati ambao hata imechelewa.

Kwa kweli japo ninazungumziwa watu wakicheka lakini ni hoja ambayo inasikitisha kwa sababu ukiangalia idara ile ya Ferry imepoteza mwelekeo Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika ukiangalia vizuri pale Ferry na tuchukue wakati kama ile Kamati ilikua yazungumziwa hapa utapata kwamba watu wetu walikua wanapata kazi; mwanzo wamechukua zile sehemu ambazo watu walikua wanatembea vizuri wakazitengeneza ma *barrier* ambayo zile sehemu leo hii Mwenyezi Mungu akileta haraka moja watu wetu hakuna mhali, wamewekwa kama jela.

Watu wamefungiwa vyuma huku na huku hawako huru wakati wanangojea Ferry, licha ya kuwa hoja hii inazungumzia watu maalum ambao ni watoto wetu lakini hoja hii Mheshimiwa nataka tungeipanua vizuri ikawa pia tunaweza kusema wale watu wetu ambao wamezaliwa katika viungo vingi wale wanaitwa *disabled* ambao wanaishi katia ulemavu fulani, hata waja

wazito wakati mwengine wanakua *mis handled* pale Ferry, kwa sababu gani? Ardhi ambayo iko pale imeweza kutumika kwa mambo mengine.

Kwa hivyo ni jukumu letu sisi kama viongozi tuangalie zile tabia anazozizungumzia Ibrahim Kondo sio jambo la leo wala jana ni la kitambo liko, watu pia wamefanya pale Ferry kama mahali ya kuhubiria watu na wengine ni sarakasi ambazo hazina heshima.

Mimi nataka nitoe mawazo yangu ya kuwa ikiwezekana huduma ile ya Ferry ni muhimu sana kwa Mombasa nzima, huduma ile kama tutaichukulia katika hali ambayo ni ya kinidhamu watu wetu watavuka katika maji ya kisawasawa kwa sababu pale kuna watu wa mikokoteni na wakati kama wanavuka hawaangalii nyuma wanaenda tu mbio mtoto wakati mwengine anagongwa.

Hali kadhalika pia ukisikia ajali zengine zinazotokea pale (??) ikirudi hakuna nafasi hata ya abiria kuweza kujitetea inabidi ile (??) ipate watu; vilevile jambo ambalo limezungumziwa pia na Mheshimwia Amur utapata kwamba yale magari katika sheria hayatakikani yavukwe yakiwa na watu sio kwamba ni pendeleo lakini ile ajali ikitokea kama ile ya Probox iliyoingia kwa maji heri afe mtu mmoja kuliko wale wote walioathirika.

Kwa hivyo hapa pia kuna uzembeaji wa kazi ambao watu fulani wanaonekama ni bora lakini wao wanahatarisha maisha ya wale wanaizuka Mheshimiwa Spika.

Mimi nataka niseme ya kwamba hoja hii ikiwezekana Mheshimiwa alieileta aende afanye utafiti zaidi akishatengeneza utafiti zaidi aitengeze kama Mswada ili wale watu tuwatajie matatizo yote; haina haja leo wameleta *parking* ili walipishe matatu na watu wetu hawako huru.

Mheshimiwa Spika sijui kama siku moja uliingia kwa vile vibanda ukapanda, maana Mheshimiwa amesema aliingia mpaka akaona hizo sarakasi zinazoendelea pale; ni kama watu ng'ombe wamewekwa katika zizi kweli, hakuna heshima wale wakianza kutoka pale hawajui mtoto hawajui mlemavu watu wanatoka mbio yule atakaebwagwa ni yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika nasema tuiangalie kwa makini na tuweze kuwaacha watu wetu waishi katika hali ya sawa, na hali ya kuheshimika kwa sababu mji wa Mombasa kila mtu anajua akifika Mombasa amefika sehemu ya kupumzika watu wanakuja kujichekea na kujivinjari.

Kwa hivyo mji wetu lazima tuulinde, ahsante sana.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Mheshimiwa wa Tononoka.

Hon. Faraj: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa fursa hii na pia kumshukuru Mheshimiwa Fadhili Mwalimu Makarani ambae kwamba ameleta taarifa ya kueleweka; taarifa ambayo ina hisia kuhusiana na watoto wetu wanaokwenda shule lutoka zile sehemu cha kivuko cha Likoni.

Mheshimiwa Spika ni lazima tupeane umuhimu pale panapotakikana umuhimu; nitatoa mfano ya kuwa leo kwa sababu ya kuweza kutunza uchumi katika sekta ya utalii tumeweza kutengeneza sheria fulani za kuweza kuwapatia wale watalii fursa ya kuendelea bila kusimamishwa na kubaki katika gari wakiwa katika kivuko na ni mihimu pia zaidi kuangalia wananchi wetu hususan watoto wetu wanaokwenda shule.

Mheshimiwa Spika mimi nataka kuunga mkono mazungumzo ambayo kwamba yamezungumzwa hapo awali kuhusiana na uchafu unaotendeka katika eneo lile la Likoni.

Mheshimiwa Spika sisi tuna watu ambao kwamba tunawawakilisha katika upande wa Tononoka ambao wanafanya vibarua Likoni na swala hili kama alivozungumzia ndugu yangu Mohamed Chiro Ndanda sio jambo geni na ni mambo yanafanyika ukweli na namuomba Mheshimiwa wa Timbwani Mheshimiwa Tom Ogalo atumie masaa yale mawili ndani ya pale.

Kwa sababu hivi vituko vinavyofanyika ni vya kila leo na ni hatari kwa watoto wetu na sisi majumbani tunawaelewa watoto wetu ili tuwapatie mustakabala mzuri lakini wakitoka pale ikiwa hatujawawekea sheria na nidhamu nzuri basi kuna watu ambao kwamba hawana misingi mema katika dunia na hua wanataka kuwabadilisha akili zao.

Pale tunapowachanganya wale wazuri na wale wabaya na watoto wetu kuna hatari kubwa wale watu wabaya kuweza kuwavuruga wale watoto na kuwabadilisha akili na ndio maana tunapata visa vingi vya ubakaji ambavyo viko Mombasa yetu na ni lazima tuchukue hatua mwafaka Mheshimiwa Spika ili kuweza kuhakikisha hili tatizo tumeliondoa na tumewapatia watoto wetu maisha na njia mwafaka anayostahili kwa mwanadamu na kwa mtoto anaeenda shule.

Lakini kuwachangaya na hao wakora, hao wahuni ambao wako pale Mheshimwia Spika kuna watu ambao wanakaa asubuhi mpaka jioni na nafikiri wanataka kupelekwa kwa daktari kwa sababu kazi wanayofanya ni kuhakikisha mwanamke yuko mbele na yeye yuko nyuma yake mpaka amalize safari yake na yake binafsi imalizike.

Kwa hivyo ni kweli haya mambo yanafanyika na kama mtu anapinga haya mambo mimi naomba sisi kama Kaunti ya Mombasa tufanye uchunguzi wetu kwa sababu wale ni watu wetu, na hatutaki wale watu wetu wapate madhara ya kiakili, wapate madhara ya kimaisha kwa sababu jambo moja katika maisha ya mtoto yanaweza kumbadilishia maisha yake yote ya mbeleni Mheshimiwa spika.

Kwa hivyo ni lazima na hili si jambo la utani wala si jambo la kucheka bali ni jambo ambalo ikiwa mimi ni mtoto wangu labda nikae *guard* na bundiki aina ya AK 47 Mheshimiwa Spika ili kusudi mtu asimsongelee karibu.

Lakini ukweli wa mambo pale pana hatari kubwa, pana ujambazi, pana uwizi, watu kila siku wanakatiwa mikoba yao kando ya wale wanaagana na wengine ambao wanaganda. Ahsante Mheshimiwa Spika.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Mheshimiwa wa Mwakirunge.

Hon. Mwinga: Ahsante sana Bwana Spika kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika mimi nisionekane ninapinga mswada huu, lakini kusema ukweli ni kwamba watu wanao vuka kivuko kile cha Likoni Ferry kufikia sasa wameongezeka; nafikiri idadi ya wale wanaovuka pale hata wafanyi kazi wenyewe wameshindwa kwa sababu watu wameongezeka, watu wamekuwa wengi.

Mheshimiwa Spika kama tunasema kwamba tukaweze kutenga ama tukaweze kuweka njia ya watoto wa shule peke yake mimi sioni hili jambo litawezekana kwangu mimi kwa sababu mimi ninavyojua pale mahali kumetengwa kwa wakina mama wana njia yao ya kupitia na wazee nao wana njia yao ya kupitia.

Sasa tukilalamika hapa tukisema kwamba wamama wetu wana dhulumiwa mahali pale mimi nakataa, kwa sababu Mheshimiwa Spika mimi nimefanya wiki moja nikiwa nalala Likoni na nikirudi huku, na Mheshimiwa Spika mimi nilikuwa mahali pale na naona wakina mama wana njia yao, ambao kina baba hawaruhusiwa kufuata ile njia. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika…

(Interruption)

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Mheshimiwa wa Shanzu.

Leader of Minority Hon. (Ms.) Maimuna Salim: Mheshimiwa Spika Mheshimiwa aliyesimama hapa anapotosha Jumba hili, hakujatengwa sehemu ya wanawake wala wanaume, sehemu ni ile ile watu wanayotembelea.

Kwa hiyo Mheshimiwa Spika tuzungumze ukweli wanaonyanyasika pale ni kina mama kwa kukojolewa na wanaume ahsante.

(Laughter)

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Mheshimiwa wa Mwakirunge?

Hon. Mwinga: Mheshimiwa Spika nafikiri Mheshimiwa wa Timbwani ungempatia nafasi aongee mwisho na huu muktadha na yeye akaweze kuuchangia, lakini nasihi jambo ambalo nataka kulisisitiza kwa sababu ya idadi ya watu ambao wameongezeka pale.

Mimi naomba kupitia Kaunti yetu hii ya Mombasa tukaweze kusaidiana pamoja na serikali kuu ili tukaweze kutoa Feri nyengine pale Mtongwe, nafikiri feri ya Mtongwe itakaporudi idadi ya watu pale Likoni itapungua na watu watakuwa wanaendelea kuvuka kama kawaida. Ahsante sana.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Mheshimiwa wa Tudor.

Hon. Siminyu: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. Mr. Speaker am glad the Chair of Transport is here and I hope a specific direction should be given so that we can visit the ferry, by the ferry management.

Mr. Speaker this has to be looked into holistically; there isn't even a chair there when a pregnant woman is moving from one area, even a sick person would stand for hours.

Mr. Speaker in fact am talking about the waiting bay, waiting bay Hon. Members there is a need of this place to be looked into and our people should be seated like in a humane manner.

Mr. Speaker I have crossed there several times, we are treated like animals, even banks nowadays have where people seat, you can't imagine where people can relax and wait, we need a place where we can relax and wait for the ferry.

Sometimes when they have mechanical problems and there is a lot of space where there can at least make improvements so that our Mombasa people can be treated in a humane manner.

Mr. Speaker Sir there is a need of this because it is very important for our women and children to be treated in the way as the culture of Mombasa people dictates; just yesterday we had a function here at our grounds here, our women were separated from men.

The culture that is now supposed to be emphasized so that they know that our women are supposed to be protected from goons Mr. Speaker Sir.

I beg this Motion at least to be directed to the relevant Committee so that they can act on it as soon as possible, thank you Mr. Speaker.

(Applause)

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Yes Hon. Rashid Nassir.

Hon. Nassir Rashid: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii, mimi kama mhusika mkubwa wa hio sehemu …

(Laughter)

Kwa sababu Ganjoni inaanza kutoka Nakumatt mpaka Makande, upande huu mimi ni mhusika mkubwa Mheshimiwa spika. Mheshimiwa Spika haya mambo yanazungumzwa ni ya kweli, na wale ambao wanapinga tutawafanyisha utafiti, tutawavalisha Madera….

(Laughter)

Mheshimiwa Spika huu mswaada ni lazima upatiwe Kamati husika, kwa sababu kuna mambo mengi sana pale; kuna wale watu walemavu, vinyanya, vibabu ambao hawajiwezi tukisema tutatenga njia zao tutafika Mama Ngina.

Mheshimiwa Spika Kamati lazima ikae chini, kwa sababu pale kuna mambo mengi; kuna kitengo ambacho tulikiomba cha kuokoa watu ambao wataongezewa kwenye feri kama itagongana ama itapenduka, kuwe kuna kikosi maalum pale na mpaka leo hakuna kikosi kama hicho hapo.

Kwa hivyo Mhehimiwa Spika hayo mambo naunga mkono, kuna mambo mengi yanatendeka pale, kina mama wanadhulumiwa sana pale, kama hawadhulumiwi kule upande wa Tom Ogalo lakini upande huu wangu wanadhulumiwa...

(Laughter)

Mheshimiwa Spika haya mambo ni ya muhimu; kina mama wanalia kweli na watoto wanalia kwa hivyo Kamati husika naomba muangalia jambo hili Kamati husika iende ikae chini isuluhishe hili jambo. Ahsante.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Mheshimiwa Mbunge Maalum Fatuma Mote.

Hon. (Ms.) Fatuma Swaleh: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii; mimi kwanza ningemshukuru Mheshimiwa Fadhili Makarani, mimi najua yeye ni kiongozi mwenye busara na ni kiongozi mwenye hekima na kiongozi ambaye alisema.

Mheshimiwa Spika mimi nimesema hivyo kulingana na Mheshimiwa anayetoka Mwakirunge alivyoongea; kwa hivyo nimempongeza Mheshimiwa aliyeleta hoja hii manake Mheshimiwa wa Mwakirunge sijui anatokea sehemu gani katika jiji la Mombasa?

Manake huko Mwakirunge mimi pia nina hakika pia kuna watu wanavuka feri sasa yeye sijui anatokea mji gani katika huu mji wa Mombasa.

Mheshimiwa Spika ni kweli kabisa sisi kina mama...

(Interruption)

Hon. Mwinga: Point of order Mr. Speaker.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Mheshimiwa wa Mwakirunge wasemaje?

Hon. Mwinga: Mheshimiwa Spika Mheshimiwa Fatuma Mote ambaye anaongea saa hii anauliza kama mimi ninatokea wapi? Mheshimiwa Spika mimi nimezaliwa Mombasa Kaunti na ninatoka Mombasa Kaunti na nimezaliwa kijiji cha Maunguja.

(Laughter)

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Yes Hon. Fatuma.

Hon. (Ms.) Fatuma Swaleh: Mheshimiwa Spika mimi nina akili yangu timamu na nimekaa na nikasikiliza wenzangu kwa makini.

Mheshimiwa Spika kumpongeza Mheshimiwa Fadhili maana ameleta hoja hii nzuri na yule Mheshimiwa anajiita ametoka Mwakirunge Mombasa Kaunti amezungumza kama ambaye hatoki Mombasa Kaunti, hatoki Mwakirunge na wala hakijui kivuko cha feri ambalo ni jambo la kusikitisha.

Mheshimiwa Spika sisi kama kina mama tunapata hujuma kubwa sana katika feri; unaweza ona mtu katika msongamano kuna wanaume ambao wana nia mbaya na sisi kina mama, kuna baadhi ya kina mama wakifika nyumbani huku nyuma mabuibui yamechafuka.

Hivyo si sawa na vile vile tungeomba pia kina mama wengi huzaa feri pale kulingana na vile wanavyosukumwa sukumwa pale utaona pengine mama amejifungua pale na vile vile tungeomba pale feri kuwe kuna mahali pengine kina mama wanaweza tengewa pengine mtu anataka kujifungua ama amejifungua kwenye feri akapata mahali pa kujihifadhi Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika ningeomba mwenye kuleta hoja hii aweze kuifanyia marekebisho kwa haraka ili tuweze kupata huduma nzuri kwenye feri. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Yes Hon. Hatimy?

Hon. Mohamed Hatimy: Ahsante sana Bwana Spika nataka tujue kuwa feri ni kampuni ya kibinafsi na nafikiri itakuwa sawa Mheshimiwa Spika kuwa kuundwe Kamati ama Kamati ya Uchukuzi waweze kwenda na nina imani yule Mwenyekiti tuliyenaye sasa ni mzee wetu tukimuita hapa atatusikiliza si kama vile ilivyokuwa mwanzo …

(Applause)

Mheshimiwa Kajembe ataweza kusikiliza kilio chetu naona Mheshimiwa Spika kama wale watu walio hapa wanajaribu kuijadili hii taarifa waweze kwenda kukaa naye na kueleza hizi shida zilioko sababu Kajembe ni mwanati wa Mombasa Kaunti na Kajembe ni mzee wetu na Kajembe ukimueleza atasikiza.

Kwa hivyo tufanyeni kwa sababu hii ni shirika la kibinafsi tukiwapelekea sheria zetu wanaweza tukataza.

Kwa hivyo ni lazima twende na sheria vile inavyotakikana lakini pia kampuni ya kibinafsi ni kuwa sisi tuwe na uhusiano mwema na wao ili kupata tuwasaidie watu wetu.

Kwa hiyo Mheshimiwa Spika naomba yule aliyeleta hii taarifa leo hapa kama ataweza kupanga asikilizane na Kamati ya Uchukuzi ili waende kukaa naye kwa haraka vile inavyotakikana na tupate yale tunayoyataka. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Yes Mheshimiwa wa Timbwani tumalizie.

Hon. Ogalo: Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika hata mimi naunga mkono hoja ambayo…

(Applause)

Mheshimiwa Fadhili ameleta lakini mazungumzo yake ni kuhusu watoto na wanawake pekee yake sababu njia iko; kuna njia ya wanawake na wanaume halafu njia ya watoto pia kuna njia huwa wanapitia lakini wakati wa kuingia wanaingia wote sasa kutoka ndio saa ile wanasukumana.

Kama ingekuwa wanaweza kutupatia feri ya watoto na wanawake pekee yake suluhisho hilo lingekuwa sawa…

(Applause)

Hapo ndio tungeongea kama Kajembe atatusukuma sukuma kupata feri moja ambayo itasimamia watoto na wanawake halafu suluhisho la hiyo feri itakuwa poa. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid)**:** Ahsante sana Mheshimiwa wa Timbwani kwa wazo lako zuri, waheshimiwa naona mmepewa muda mwingi na mkalizungumza kwa kina jambo hili na kwa mtazamo wangu waheshimiwa wengi walikuwa wakisema kwa pamoja na Mheshimiwa Fadhili kuwa watoto wananyanyaswa na si watoto pekee hata mama zetu wananyanyaswa na kuibiwa mapenzi yao hilo si jambo jema.

Kwa hiyo ningesema Mwenyekiti wa Kamati ya Uchukuzi na Ubebaji wakishirikiana na aliyeleta hoja hii kama si Mwanachama wa Kamati hiyo ningependa mumchukue kwa sababu ni *interested party* na muende mukamtembelee Mwenyekiti wa Feri ili muweze kutatua suala hili na nawapatia wiki mbili halafu murudishe majibu kwa hii Nyumba. *Yes Clerk.*

ADJOURNMENT

There being no other business members this House stand adjourned until tomorrow in the afternoon.

The House rose at 3.21pm.